



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (alijeshika fimbo) akiwaongoza ng'ombe kwenda kwenye joshu la Kijiji cha Kinango Wilaya ya Magu mkoani Mwanza wakati wa zoezi la kuogesha mifugo. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

HABARI LEO / A

31/12/2020

B
a
k
Na
I
sa
kw
ka
eli
kw
ha
Ki
mk
hiy
ina
wa
sha
kur
wat
tuel
kati
miu
uka
alisa
kifu
shal
sabu
za
wah

Bodi ya Maziwa yajipanga kuimarisha masoko

Na Mwandishi Wetu

■ ■ KAIMU Msajili wa Bodi ya Maziwa, Noely Byamungu amesema bodi hiyo imejipanga kuimarisha masoko ya maziwa na bidhaa zake, ili kuongeza usindikaji wa maziwa unaoitanywa chini ya kiwango na viwanda vya maziwa nchini.

Aliyasema hayo juzi jiji Dar es Salaam wakati alipotembelea kiwanda cha maziwa cha Milkcom Dairies lilichopo Kigamboni jiji Dar es Salaam kwa lengo la kuingalia namna bora ya ushikishwaji wa wasindikaji maziwa katika mpango wa majaribio wa Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni na unywaji wa maziwa kwenye ofisi za senkai.

Kiwanda cha Milkcom, kinasindika takribani lita 20,000 za maziwa chini ya uwezo wa kiwanda uliosimikwa wa kusindika lita takribani 100,000 kwa siku.

Byamungu alisema kuwa Bodi ya Maziwa, ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji wa Mpango wa Majaribio wa Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni, utakaanza hivi karibuni katika mkoa mbalimbali nchini utakaomimarisha masoko ya maziwa kwa wenye viwanda.

Alisema mpango huo, utasaidia viwanda kupata masoko ya maziwa kwa wingi lakini pia kuimarisha afya ya mwili na akili za watoto pindi wawapo darasani na hivyo kuongeza utafu wa warafuzi.

Sanjani na hilo, Byamungu alisema Bodi ya Maziwa itahakikisha Ofisi za Senkai zinakuwa wanunzi wakubwa wa maziwa kwa kutumia maziwa yanayozalishwa ndani ya nchini, ili kuongeza unywaji wa maziwa ambapo kwa sasa wastani wa unywaji maziwa kwa mtu kwa mwaka ni lita 54.7 pekee kulinganishwa na lita 200, zinazopendekezwa na Shirika la Afya Dunia (WHO) pamoja na FAO.

Kaimu Msajili huyo alisema, ongezeko la unywaji wa maziwa litasaidia kuimarisha kipato cha mfugaji na kuimarisha uchumi wa viwanda vya ndani.

Naye Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Milkcom, Abubakar Faraji alisema usindikaji huo mdogo umesababishwa na miundombinu mibovu ya uzalishaji maziwa, ikiwemo barabara pamoja na umeme vinavyosababisha kiwanda kusindika maziwa chini ya uwezo wake.

Faraji alisema kukatika kwa umeme mara kwa mara na kwa muda mrefu, kunaisababishia kampuni hasara kwani hulazimika kutumia jenereta katika usindikaji wa maziwa, ili kuepuka hasara ya maziwa kuharibika.

"Kutokana na changamoto hiyo, kampuni imejika kutumia gharama kubwa za uendeshaji wa bashara ya maziwa kuliko ilivyotarajiwa na hivyo kusindika chini ya uwezo wake," alisema.

Alitaka Bodi ya Maziwa, kuja na mikakati itakayosaidia wasindikaji kupata masoko ya maziwa ili kuweza kuzalisha maziwa kwa wingi, ikiwemo kutoa hamasa kwa wananchi kupita yombo vya habari juu ya maziwa na hatimaye unywaji wa maziwa na bidhaa zake nchini.

From DAILY NEWS Reporters in Dodoma

Support looms fo

THE new leaders of the Tanzania Women Miners Association (TAWOMA) have pledged to boost income of women engaged in mining activities countrywide.

They made the pledge after they were elected to lead the organization for the next five years in a tenure that ends in 2025.

The election that was recently conducted in Dodoma, saw Ms Gilly Raja emerging victorious as the new chairperson, replacing Ms Eunice Ngele, who led the associa-

tion for the past five years.

Elaborating, they also pledged to address challenges facing women miners in a bid to help them improve their livelihoods and as well boost the country's economy.

The election also saw Ms Salma Kundy being elected as their new Secretary General.

However, speaking after the election Ms Raja said it was time to help women so that they fight poverty, adding that the sector contributes immensely to the country's

economy.

Currently, the n sector's contribution to Gross Domestic P (GDP) is estimated at cent.

"Our intention a leaders is to lift wom poor to higher status through mining," sl noting that there wa to increase value mining activities e gemstones in the co

To ensure that T seek a market in th sector for the wome

Use TALIRI centre for improved livestock keeping, herders told

PASTORALISTS in Dodoma and neighbouring regions have been advised to effectively use pieces of advice from the Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI) to further improve their livestock keeping activities.

Making the appeal, a researcher at TALIRI Mpwapwa Centre, Erick Mbisha, during a media tour organized by the Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH) to Mpwapwa district, recently said herds should use the centre for modern crossbreeding in order to obtain hybrid offspring.

Mr Mbisha further noted that some reared livestock known as Mpwapwa cattle at the centre is the best breed for them because, they can live in any environment, grow

fast and can produce enough meat, besides being resistant to several diseases.

"Many of them have been sending messages of appreciation that the Mpwapwa cattle can live in any environment and that they are drought resistant," said the researcher.

He said their survey and conducted research found that the breed selection is also suitable for the tropical environments.

Elaborating, he said pastoralists should acquire and maintain parent genetic materials from them.

According to Mr Mbisha at their Iloilo area cattle farm, many pastoralists have been flocking the area to buy their products, because they have proved to raise their breeds.



**A FOOD
minimize**

Ndaki awataka wafugaji kuzalisha mifugo yenye ubora

Na Edward Kondela, Mwanza

■ ■ WAFUGAJI wametakiwa kuanza kufikira kuwa na ng'ombe bora badala ya kuwa na ng'ombe wengi wasio na ubora ambao hawakidhi tija katika maisha yao kwa kutotaa mazao bora ambayo hayawezi kutoa kipato cha kukidhisha.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Kinango kilichopo Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza wakati akishuhudia zoezi la uogeshaji mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani humo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki amesema mifugo mingi wakiwemo ng'ombe ni njia mojawapo ya kutunza fedha ambayo imekuwa ikitumiwa na wafugaji hivyo ni muhimu wafugaji hao kuhakikisha mifugo yao inakuwa bora.

"Nchi yetu tuna ng'ombe wengi sana, lakini wengi siyo bora kama inavyotakiwa sasa tunatakiwa kutoka kuwa na ng'ombe wengi tu bali tuwe na ng'ombe walio bora, tukiwa na ng'ombe wengi wasio bora hawatusaidii sana katika

maisha yetu, kwa sababu lengo la kuwa na ng'ombe atupe nyama, atupe maziwa na atupe kipato sasa tufikirie kuwa na ng'ombe bora na moja ya njia ya kuwa na ng'ombe bora ni hi ya kuwatogetsha," alisema Ndaki.

Ndaki aliongeza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 imetenga bajeti ya kukarabati majosho kadhaa yaliyopo maeneo mbalimbali nchini na kuahidi kuwa wizara itakarabati majosho matano yaliyopo katika Wilaya ya Magu ili mifugo mingi iweze kuogeshwa na kuwa bora.

Pia, Waziri Ndaki aliambatana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Pauline Gekul katika ziara hiyo amesema njia nyingine ya kuwa na ng'ombe bora ni wafugaji kuhakikisha mifugo yao inapata malisho bora ambayo yatafanya mifugo hiyo kuwa na aya bora lakini kwa sasa wafugaji wamekuwa wakichunga katika maeneo machache hali inayofanya mifugo kutokula chakula kinachotakiwa.

Aliongeza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishughulika sana suala la malisho ambalo ni moja ya tatizo kubwa kwa wafugaji

pamoja na maji na kutumia fursa hiyo kumshukuru Rais Dkt. John Magufuli kutokana na kuruhusu wafugaji wachunge kwenye baadhi ya maeneo yaliyokuwa ya hifadhi na mengine kuzuliwa hali iliyotoa ahueni kwa wizara kupata maeneo ya kulisha mifugo ili iwe na ubora.

Kwa upande wake Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Nchini (TMB) Iman Sichahe amewaeleza wafugaji kuwa suala la kuogeshwa mifugo dhidi ya magonjwa ni muhimu kwa kuwa imekuwa likizua Tanzania kuuza nyama katika nchi mbalimbali kutokana na viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama kutopata mifugo bora.

Alifafanua kuwa uogeshaji unaboresha aya ya mifugo ikiwemo ya nyama na ngozi hivyo kuitanya viwanda kufanya kazi na kuwaongezea vipato wananchi kwa kupata masoko ya kuuza mifugo yao, serikali kupata fedha kupitia tozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi bora.

Katika ziara hiyo Waziri Ndaki alitembelea pia kiwanda cha kuchinja na kuchakata nyama cha Alpha Choice kilichopo wilayani

Magu na kuzungumza na baadhi ya wafugaji waliofika kiwanda hapa kwa kuwataka waanze kubadilisha ubora wa mifugo yao kwa kuwapata maji na malisho yanayotosheshesha na kuacha kuwachunga katika maeneo marefu ili mifugo hiyo iwe na aya nzuri.

Ndaki alisisitiza hilo baada ya kupata malalamiko kutoka kwa baadhi ya wawekezaji kwenye viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama kutopata ng'ombe bora ambao wanaweza kukidhi katika soko la kimataifa hali ambayo wakazi mwingine nyama kukataliwa na baadhi ya nchi kutokana na mifugo kuwa na magonjwa na nyama kutokuwa na ubora unaoitakiwa.

"Nawaombeni sana tuanze kuboresha ng'ombe wetu ili tupate faida ya kuwa na kiwanda hapa na kingine nimekiona kule waziyani Misungwi na chenyewe wanapata ng'ombe kidogo sababu ni hii hiiyo ng'ombe wetu hawajawa bora sana, sasa wawekezaji hawa wamelezimika wawe wananunua ng'ombe wanawafuga mahali kwanza wanawalisha ili wabadilike sura na aya waliyotoka nayo kwa wafugaji," alifafanua Ndaki.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki akizungumza na baadhi ya wafugaji (hawapo pichani) waliofika katika kiwanda cha kuchinja na kuchakata nyama, Alpha Choice kilichopo Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, ambapo amewataka wabadili fikra za ufugaji na wafuge kisasa ili wapate ng'ombe bora. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul kulia kwake ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah. Waziri Ndaki amemaliza ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Mwanza (Picha na Edward Kondela- Wizara ya Mifugo na Uvuvi)

Waziri Mashimba asisitiza ufugaji wa ng'ombe bora

NA MWANDISHI WETU,
Mwanza

WAFUGAJI wametakiwa kuanza kufikiria kuwa na ng'ombe bora, badala ya kuwa na ng'ombe wengi wasio na ubora, ambao hawakidhi tija katika maisha yao kwa kushindwa kutoa mazao bora yanayoweza kutoa kipato cha kuridhisha.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alipozungumza katika Kijiji cha Kinango, kilichopo Wilaya ya Magu, Mkoani Mwanza.

Waziri Mashimba, aliyasema hayo alipokuwa akishuhudia uogeshaji mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali alipokuwa katika ziara ya siku mbili mkoani humo.

Mashimba, alisema mifugo mingi, wakiwemo ng'ombe ni njia mojawapo

ya kutunza fedha, ambayo imekuwa ikitumiwa na wafugaji, hivyo ni muhimu kuhakikisha mifugo yao inakuwa bora kwa kuipatia huduma muhimu, ikiwemo ya kuiogesha.

Nchi yetu tuna ng'ombe wengi sana, lakini wengi siyo bora kama inavyotakiwa, sasa tunatakiwa kutoka kuwa na ng'ombe wengi, tuwe na ng'ombe walio bora.

"Tukiwa na ng'ombe wengi wasio bora, hawatusaidii sana katika maisha yetu, kwa sababu lengo la kuwa na ng'ombe atupe nyama, atupe maziwa na atupe kipato, sasa tufikirie kuwa na ng'ombe bora na moja ya njia ya kuwa na ng'ombe bora ni hii ya kuwaogesha," alisema.

Mashimba, aliongeza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imetenga bajeti

ya kukarabati majosho kadhaa yaliyopo maeneo mbalimbali nchini na kuahidi wizara itakarabati majosho matano yaliyopo katika wilaya ya Magu, ili mifugo mingi iweze kuogeshwa na kuwa bora.

Akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, alisema njia nyingine ya kuwa na ng'ombe bora ni wafugaji kuhakikisha mifugo yao inapata malisho bora, ambayo yatafanya mifugo hiyo kuwa na afya bora.

"Kwa sasa wafugaji wamekuwa wakichunga katika maeneo machache, hali inayofanya mifugo kutokula chakula kinachotakiwa," alisema.

Alimshukuru Rais Dk. John Magufuli, kutokana na kuruhusu wafugaji wachunge kwenye baadhi ya maeneo yaliyokuwa hifadhi

na mengine kuzulliwa, hali iliyotoa ahueni kwa wizara kupata maeneo ya kulisha mifugo ili iwe na ubora.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Iman Sichelwe, aliwaeleza wafugaji kuwa suala la kuogesha mifugo dhidi ya magonjwa ni muhimu kwa kuwa limekuwa likizuia Tanzania kuuza nyama katika nchi mbalimbali kutokana na viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama kutopata mifugo bora.

Alifafanua kuwa uogeshaji unaboresha afya ya mfugo, ikiwemo ya nyama na ngozi, hivyo kuvifanya viwanda kufanya kazi na kuwaongezea vipato wananchi kwa kupata masoko ya kuuza mifugo yao, serikali kupata fedha kupitia tozo mbalimbali na upatikanaji wa fedha za kigeni.

Uhum, 8 31/12/2020